

Tell: 2533015 au 2533016  
Fax: 027-2533016  
Email: md@mbuludc.go.tz  
Mbulu-Manyara



Mkurugenzi Mtendaji (W)  
S.L.P 74  
MBULU.

## TANGAZO LA ZABUNI KUWAPATA MAWAKALA WA UKUSANYAJI WA USHURU KWA KIPINDI CHA KUANZIA JULAI 2017 HADI JUNI 2018

26/04/2017

Halmashuri ya Wilaya ya Mbulu katika mwaka wa fedha 2017/2018 inakusudia kukusanya mapato katika vyanzo vyake mbalimbali kwa mkataba wa miezi kumi na mbili (12) kuanzia tarehe 01/07/2017 hadi tarehe 30/06/2018. Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu inawatangazia wananchi, Makampuni na Taasisi mbalimbali kuleta maombi ya zabuni za uwakala wa kukusanya ushuru kama ifuatavyo;

AINA YA ZABUNI	NAMBA YA ZABUNI
Wakala wa kukusanya ushuru wa Mifugo Mnadani, Ushuru wa soko Mnadani na Ushuru wa Machinjio Mnadani: <ol style="list-style-type: none"><li>1. Mnada wa Maghang</li><li>2. Mnada wa Maretadu</li><li>3. Mnada wa Dongobeshi</li><li>4. Mnada wa Dirim</li><li>5. Mnada wa Masqaroda</li><li>6. Mnada wa Kidarafa</li></ol>	LGA/061/2017-18/HQ/01

### 2 USHURU WA MAZAO

Mahindi, Maharage, Dengu, Alizeti, Ulezi, Ngano, Kahawa, Vitunguu Maji, Vitunguu Swaumu, Njegere, Viazi Mviringo, Pareto, Atmisia na mazao mengine yanayopatikana na kuuzwa Mbulu.	LGA/061/2017-18/HQ/02
--	-----------------------

### 3. USHURU WA STENDI

1. Ushuru wa stendi Dongobesh 2. Ushuru wa stendi Haydom	LGA/061/2017-18/HQ/03
---	-----------------------

### 4. USHURU WA MACHINJIO

1. Ushuru wa Machinjio wa kila siku – Dongobeshi Mjini	LGA/061/2017-18/HQ/04
2. Ushuru wa Machinjio wa kila siku -Haydom Mjini	LGA/061/2017-18/HQ/05

### 5 USHURU WA VYOO VYA KULIPIA KATIKA STENDI YA HAYDOM NA DONGOBESHI

1.Ukusanyaji wa ushuru wa choo cha kulipia katika stendi ya Haydom. 2. Ukusanyaji wa ushuru wa choo cha kulipia katika stendi ya Dongobesh.	LGA/061/2017-18/HQ/06
--	-----------------------

### 6: USHURU WA MABANGO

Ukusanyaji wa ushuru kwenye mabango yote ya biashara Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu.	LGA/061/2017-18/HQ/07
--	-----------------------

## **MASHARTI YA KUOMBA ZABUNI ZA UWAKALA WA MAPATO.**

1. Nyaraka za zabuni zinapatikana kwa kulipa ada ya **shilingi 100,000** (Laki moja) kwa kila Zabuni. Nyaraka za Zabuni zinapatikana kwenye ofisi ya manunuzi na ugavi, Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu.
2. Zingatia kuwa fomu ya maombi ya Zabuni inajazwa na kusainiwa na mwenye uhalali wa kisheria (Power of Attorney) katika zabuni hii.
3. Mwombaji wa Zabuni ya ukusanyaji wa mapato endapo atachaguliwa, atalazimika kuilipa Halmashauri fedha taslimu ambayo ni dhamana ya kazi anayopewa kabla ya kuanza kazi. Kiwango cha dhamana ni sawa na makusanyo ya miezi mitatu ya zabuni husika. **Mshindi wa zabuni hataruhusiwa kuanza kazi ya kukusanya ushuru kabla ya kulipa fedha yote ya dhamana.**
4. Mwombaji awasilishe zabuni halisi na nakala mbili.
5. Zabuni ijazwe vizuri, iwekwe kwenye bahasha iliyofungwa kwenye bahasha baada ya **kujazwa na wazabuni** na juu ya bahasha iandikwe kwa **HERUFI KUBWA ZABUNI ILIYOOMBWA** bila kuwekwa alama yoyote ya kumtambulisha muombaji.
6. **Mwombaji asiwe mtumishi wa Serikali/Shirika la Umma.**
7. Zabuni zitawasilishwa kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, makao makuu ya Halmashauri, ofisi ya manunuzi na ugavi.
8. **Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe 10.05.2017 saa nne kamili asubuhi**, na zabuni zitafunguliwa ndani ya dakika 30 baada ya muda wa kuwasilisha zabuni kuisha.
9. Zabuni zote ziambatane na kiapo cha dhamana ya zabuni (Tender securing declaration) kwa kuzingatia fomati ilioainishwa katika kitabu cha zabuni.
10. Waombaji wanakaribishwa kuhudhuria wakati wa ufunguzi katika ukumbi wa mikutano wa Halmashauri uliopo makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya.
11. Zabuni ambazo zitachelewa kwa muda uliopangwa na zabuni zitakazotumwa kwa mtandao (e-mail, fax) hazitapokelewa.
12. Halmashauri hailazimishwi kwa njia yoyote kukubali ombi lolote.
13. **Mwombaji aandike barua ya maombi ya zabuni** na kuiwasilisha kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, ofisi ya manunuzi na ugavi, Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, S.L.P 74,Mbulu.
14. Mwombaji atakayeshindwa masharti haya atakuwa amejiondoa mwenyewe kwenye mchakato mzima wa zabuni.

**Hudson S. Kamoga  
Mkurugenzi Mtendaji  
Halmashauri ya Wilaya Mbulu.**